

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 5 WA WANAHISA WA BENKI

- 5.1 Taarifa inatolewa kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 5 wa Mwalimu Commercial Bank Plc utafanyika katika Ukumbi wa LUSH GARDEN HOTEL – Arusha Mjini siku ya Ijumaa, Oktoba 22, 2021 kuanzia saa 5:00 Asubuhi
- 5.2 Ajenda za Mkutano ni kama ifuatavyo:
 - 5.2.1 Kufungua Mkutano
 - 5.2.2 Kupitisha dondoo za Mkutano.
 - 5.2.3 Uthibitisho wa Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 4 wa Mwaka 2020
 - 5.2.4 Kujadili yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa 4 wa mwaka 2020.
 - 5.2.5 Taarifa ya Mwenyekiti
 - 5.2.6 Kupokea Ripoti ya Wakurugenzi na kupitishwa kwa taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka ulioishia 31 Disemba 2020.
 - 5.2.7 Azimio la Gawio kwa mwaka 2020
 - 5.2.8 Taarifa ya hatua iliyofikiwa katika kuongeza mtaji wa Benki
 - 5.2.9 Kupokea na kuidhinisha Malipo ya Wakurugenzi
 - 5.2.10 Kupokea na kuthibitisha Uteuzi wa Mkaguzi wa nje wa Hesabu kwa mwaka unaoishia 31 Disemba 2021
 - 5.2.11 Mengineyo yatokanayo na mkutano
 - 5.2.12 Tarehe ya mkutano ujaa
 - 5.2.13 Kufungwa kwa Mkutano
- 5.3 Mwanahisa yeyote ambaye anataka kuingiza pendekezo lake katika kipengele cha 5.2.11 hapo juu lazima atoe taarifa kwa maandishi siku tatu (3) kabla ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.
- 5.4 Mwanahisa atakayeshindwa kuhudhuria, ana haki ya kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano kwa nia-ba yake. Taarifa hizi zimfikie Katibu angalau saa arobaini na nane (48) kabla ya wakati wa mkutano.
- 5.5 Wanahisa wote wanaombwa kuja na vyeti vya hisa pamoja na vitambulisho siku ya mkutano.
- 5.6 Makabrasha ya mkutano yanapatikana kwenye matawi yetu ya Samora Avenue na Mlimani Tower Dar es Salaam, na katika ofisi zetu za Arusha, Dodoma, Mwanza, Morogoro na Mbeya. Pia yatapatikana kwenye ukumbi siku ya mkutano na kwenye tovuti ya benki kuanzia tarehe 15/10/2021.
- 5.7 Gharama za usafiri na malazi zitafanywa na wanahisa wenyewe.

Mwalimu Commercial Bank Plc

TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu “Hisa”, “Elimu ya Fedha na Bidhaa zinazotolewa na Benki ya Mwalimu. Semina hiyo itafanyika Ijumaa, tarehe 22/10/2021 katika Ukumbi **LUSH GARDEN HOTEL, SAKINA** – Arusha Mjini kuanzia saa 3.00 asubuhi.